





# UMOJA
# UN Tanzania

Toleo Na. 82
Januari - Februari 2019


## Kamishna wa UNHCR atembelea Tanzania



Kamishna Mkuu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kushughulikia Wakimbizi (UNHCR), Bw. Filippo Grandi (kulia) akutana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mh. Dkt. John Joseph Magufuli (kushoto). Nyuma yake ni Waziri wa Katiba na Mambo ya Sheria, Mh. Dkt. Augustine Mahiga. ***Picha | UNHCR***

### Vidokezo

- Shirika la mazingira la UN lahimiza kukabili uchafuzi wa mazingira kwa plastiki kupitia 'Flipflopi'
- Ripoti maalumu: Norway yatoa $7millioni katika Programu ya Pamoja ya Kigoma katika kukomesha ukatili wa wanawake na watoto
- Vijana wasisitiza Ukeketaji ukomeshwe

Mapema mwezi Februari, Kamishna Mkuu wa Shirika la Kuhudumia Wakimbizi, Bw. Filippo Grandi, alizuru Tanzania na kuhitimisha ziara yake hiyo kwa kutoa wito wa kufanya uwekezaji zaidi katika Mkoa wa Kigoma ambako wakimbizi wapatao 330,000 wanaotoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Burundi kwa sasa wanahifadhiwa. Akiitaja Tanzania kama "moja ya nchi muhimu sana zinazotoa hifadhi kwa wakimbizi barani Afrika," Bw. Grandi alieleza kuridhishwa kwake na ahadi ya serikali kwamba Tanzania itaendelea kuwapokea wakimbizi.

Katika mkutano wake na Rais John Pombe Magufuli, Bw. Grandi aliipongeza Tanzania kwa utamaduni wake wa muda mrefu wa kutoa hifadhi kwa wakimbizi wanaokimbia machafuko na utesaji katika nchi za jirani, ikiwemo hatua ya Tanzania ya

*Inaendelea ukurasa wa 2*

### Kauli ya Serikali

***"Ningependa kutoa shukrani zangu za dhati kwa Norway kwa mchango wa fedha ili kusaidia Programu ya Pamoja ya Kigoma (KJP). Tunashukuru sana kwa ukarimu huu na tutaendelea kushirikiana na Umoja wa Mataifa katika kuleta maisha bora ya wanajamii katika mkoa huu."***

**Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Brigedia Jenerali (Mstaafu) Emmanuel Maganga, alipokuwa akizunguza katika mkutano wa pili wa Kamati ya Uongozi ya Programu ya Pamoja ya Kigoma uliofanyika Kigoma Mjini, mnamo tarehe 25 Januari, 2019.**

*Inatoka ukurasa wa 1*

kuwapa uraia wakimbizi 162,000 waliokimbia Burundi mwaka 1972. Kamishna huyo mkuu aliahidi kutoa misaada zaidi ili kuendeleza jitihada za kiutu na pia kuleta maendeleo kwa jamii za wenyeji, kuimarisha usalama kwenye makambi na kusaidia miradi ya ulinzi wa mazingira, hasa kwenye vyanzo vya nishati vilivyo mbadala wa kuni. Wakuu hawa wawili walizungumzia kuanzishwa kwa mifumo ya kisheria ya kikanda ambayo itasaidia kuimarisha maisha na kutafuta ufumbuzi wa yanayowasibu wakimbizi kutoka Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Katika miaka miwili iliyopita, jumla ya wakimbizi 57,865 kutoka Burundi wamesaidiwa kurejea nchini kwao. Bw. Grandi aliielezea Tanzania kama nchi yenye utulivu mkubwa katika ukanda wenye machafuko mengi na aliipongeza kwa kazi inayofanya ya kuleta amani na kuwaomba viongozi wa nchi kuendeleza jitihada hizo.

Asilimia 74 ya wakimbizi na watafuta hifadhi wanaoishi nchini Tanzania wanatoka Burundi, na asilimia 26 wanatoka katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Walio wengi wanaishi katika kambi zilizo jirani na mpaka na wengi wao wameishi hapo kwa miongo kadhaa. Bw. Grandi aliisifu Tanzania kwa kuunga mkono Ushirikiano wa Kimataifa kwa ajili ya Wakimbizi, ambayo ni makubaliano yanayohimiza mshikamano zaidi miongoni mwa jamii ya kimataifa inayotoa hifadhi kwa wakimbizi.



Kamishna Mkuu wa UNHCR, Bw. Filippo Grandi (kushoto) akijadiliana jambo na Waziri wa Katiba na Mambo ya Sheria, Mh. Augustine Mahiga (kulia). ***Picha | UNHCR***

## Shirika la Mazingira la UN lahimiza juhudi za kukabili uchafuzi wa mazingira kwa plastiki kupitia 'Safari ya Flipflopi'



Mtoto akishiriki katika kazi ya kusafisha fukwe katika eneo la Bustani za Forodhani katika Mji Mkongwe wa Zanzibar. Serikali, Umoja wa Mataifa, makundi mbalimbali ya vijana na wadau wengine walishiriki katika kazi hiyo ya usafi. ***Picha | Zainul Mzige***

Mapema mwezi Februari, 2019, mashua iliyotengenezwa na kupambwa kwa "kandambili" (Flipflopi) ilitweka Tanga kutoka Kenya na kufanya safari ya kihistoria ya kilometa 500 kutoka katika Kisiwa cha Lamu, nchini Kenya, hadi Mji Mkongwe, Zanzibar, nchini Tanzania. Mashua hiyo ambayo imetengenezwa kwa plastiki zilizoundwa upya, ilibatizwa jina hilo kutokana na kuundwa kwa takribani vipande 30,000 elfu vya kandambili pamoja na takataka nyingine za plastiki. Takataka hizo zilitokana na uchafu uliokusanywa kutoka kwenye fukwe za bahari baada ya kampeni ya usafi katika mwambao wa Kenya.

Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira lilishirikiana na mwanzilishi, Bw. Ben Marison, ambaye alihamasishwa na kupata wazo la kuunda mashua hiyo mwaka 2016 baada ya kuona jinsi taka za plastiki zilivyoenea katika pwani ya Kenya.

*Inaendelea ukurasa wa 3*

*Inatoka ukurasa wa 2*

Msaada wa Shirika la UN la Mazingira katika ziara hii ya 'Flipflopi' unaangukia katika Kampeni ya Safisha Bahari, ambayo inalenga kuzihimiza serikali, umma, vyombo vya habari, vyama vya kiraia na sekta binafsi kupambana na uchafuzi wa mazingira ya bahari kwa plastiki.

Safari ya kilometa 500 kutoka Lamu ililenga kukuza uelewa kuhusu tani milioni 8 hadi 12 za taka za plastiki zinazotupwa baharini kote ulimwenguni kila mwaka. Katika safari yake hiyo, mashua hiyo ilitua Tanga katika miji sita ya Kenya na Tanzania, na kutoa elimu kuhusu uchafuzi wa bahari. Elimu hiyo iliwalenga wanajamii wanaoishi mwambao, shule na maofisa wa serikali.

Safari hiyo ya 'Flipflopi' ilipokelewa na Rais wa Kikao cha Nne cha Baraza Kuu la Shirika la Umoja wa Mataifa (UNEA-4), Bw. Siim Valmar Kiisler, aliyeambatana na maofisa wa ngazi za juu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, akiwemo Makamo wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mh. Balozi Seif Ali Iddi; Mheshimiwa Mohamed Aboud Mohamed, Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais anayeshughulika na mazingira; Bw. Khatib Abdulrahman Khatib, Meya wa Mji Mkongwe; watumishi wa ofisi za kibalozi na pia Mratibu Mkazi wa Umoja wa Mataifa, Bw. Alvaro Rodgriguez, pamoja na wawakilishi wa Shirika la UN la Mazingira na Shirika la Maendeleo la UN (UNDP).

Baada ya kutembelea Zanzibar, kampeni hiyo ya 'Flipflopi' ilielekea hadi mji mkuu wa Kenya, Nairobi, ambako Wakuu wa Nchi, mawaziri wa mazingira, wanaharakati wa mazingira, wabunifu, mashirika yasiyo ya kiserikali na wakurugenzi wakuu wa makampuni ya kimataifa walikutana hivi karibuni kwa ajili ya mkutano wa UNEA-4, ambao ni jukwaa muhimu kabisa duniani kuhusu masuala ya mazingira.



Mashua iliyoundwa kwa Kandambili ('Flipiflopi') ilipokuwa ikiwasili katika Bandari ya Zanzibar baada ya kusafiri kilomita 500 kutoka Lamu, Kenya. Mashua hiyo imetengenezwa kwa kutumia takribani kandambili 30,000 zilizotumika. ***Picha | Zainul Mzige***

## Siku ya Kupinga Ukeketaji




Faidha Yusufu, Mratibu wa Dawati la Jinsia na Watoto katika Jeshi la Polisi, akizungumza na wanafunzi wa shule za msingi na sekondari na wadau wengine katika Mkoa wa Mara kuhusu Siku ya Kimataifa ya Kutovumilia Kabisa Ukeketaji (FGM). ***Picha | UNFPA Tanzania/Warren Bright***

Maadhimisho ya mwaka huu ya Kimataifa ya Kutovumilia Kabisa Ukeketaji Wanawake (FGM) yalifanyika katika Wilaya ya Tarime, Mkoa wa Mara. Maadhimisho hayo yaliongozwa na mashirika ya Msichana Initiative, Hope for Girls and Women, Tanzania, na ATFGM-Masanga, kwa ufadhili wa Mfuko wa Umoja wa Mataifa wa Idadi ya Watu (UNFPA), Ubalozi wa Umoja wa Ulaya nchini Tanzania, Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, Plan International na Terre des Hommes. Vijana kutoka

*Inaendelea ukurasa wa 4*

*Inatoka ukurasa wa 3*
katika wilaya tatu za mkoa wa Mara zikiwemo Tarime, Butiama na Serengeti waliungana na kutoa wito kwa sauti moja kwa serikali ili kuwaunga mkono katika juhudi zao za kukomesha ukeketaji.

Mkuu wa Mkoa wa Mara, Bw. Adam Malima, aliitikia wito huo na kutangaza kwamba atatumia madaraka yake kuwalinda wasichana dhidi ya ukatili wa ukeketaji. Kwa upande wake, Faidha Suleiman, ambaye ni Mratibu wa Taifa wa Madawati ya Jinsia na Watoto katika Kituo cha Polisi, alisema kwamba matokeo ya ahadi ya Polisi na msaada unaotolewa na UNFPA, hatua kubwa imepigwa katika kushughulikia kesi zinazohusiana na ukeketaji.
UNFPA nchini Tanzania inaendelea kuunga mkono juhudi za serikali za kukomesha ukeketaji kupitia mpango wa muda mrefu unaojulikana kama Mpango wa Taifa wa Kuchukua Hatua za Kukomesha Vitendo vya Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto wa 2017/2018 hadi 2021/2022.

Msaada wa UNFPA kwa Polisi Tanzania umejenga uwezo wa maofisa kubaini na kuchukua hatua dhidi ya matukio ya ukeketaji; Madawati ya Jinsia na Watoto yameimarishwa na maofisa wamepata mafunzo kuhusu vitendo vya ukatili wa kijinsia ambao unajumuisha pia ukeketaji (FGM). Kujenga uwezo wa Kituo cha Msaada kwa Watoto (National Child Helpline) kumeongeza mahitaji ya huduma na ufanisi zaidi katika kushughulikia masuala ya ukeketaji.

Vilevile, UNFPA imeendelea kuratibu programu za unyago mbadala zinazoendeshwa na Chama cha Kukomesha Ukeketaji cha Masanga (ATFGM) cha Wilayani Tarime, na Hope for Girls and Women (Matumaini kwa Wasichana na Wanawake), Tanzania wilayani Butiama na Serengeti, ambavyo vinatoa utaratibu mbadala kwa "ukeketaji" ili kuashiria safari ya kukua kutoka utoto kuingia utu uzima kwa msichana. Mwaka 2018, jumla ya wasichana 801 walikingwa dhidi ya ukeketaji kupitia programu hizi za unyago mbadala kwa usimamizi wa ATFGM-Masanga na Tumaini kwa Wasichana na Wanawake.

Kwa kutoa misaada kwa wizara zinazohusika na washirika wengine, UNFPA imedhamiria kuhakikisha kwamba hadi kufika mwaka 2030 hakutakuwa na msichana anayeishi kwa kuogopa kukeketwa nchini Tanzania. Viongozi wa dunia kwa kauli moja waliungana na kupitisha suala hili kama moja ya malengo ya Ajenda ya 2030 kwa malengo ya kukomesha ukeketaji. Hatua kadhaa zimepigwa nchini Tanzania na ukeketaji umepungua lakini kama nchi haina budi kuongeza juhudi ili kufikia lengo hilo.




Wasichana wakisherehekea Siku ya Kimataifa ya Kutovumilia Kabisa Ukeketaji iliyoandaliwa na Hope for Girls and Women, katika Wilaya ya Serengeti, Mkoa wa Mara. ***Picha | UNFPA Tanzania/Warren Bright***

# Umoja wa Mataifa, Serikali na Wadau wa Vyombo vya Habari waadhimisha Siku ya Redio Duniani huko Tanga




Mwakilishi wa Nchi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO), Mr. Tirso Dos Santos, akizungumzia uzoefu wake kuhusu umuhimu wa redio katika harakati za ukombozi wa Afrika. ***Picha | UNESCO***

Maadhimisho ya Siku ya Redio Duniani yalikuwa yenye mafanikio makubwa ambapo serikali, Umoja wa Mataifa na wadau wa vyombo vya habari waliahidi kuendelea kusukuma maendeleo ya upashanaji habari nchini Tanzania, hasa kwa upande wa redio. Maadhimisho hayo yalifanyika Tanga katikati ya mwezi Februari na yaliongozwa na UNESCO kwa ushirikiano na mtandao wa vyombo vya habari vya jamii—TADIO.

Changamoto zilizoibuliwa na TADIO, ambayo ina jumla ya vituo vya redio wanachama 25, ziligusa masuala ya gharama kubwa za uendeshaji huku vituo hivyo vya redio vikiwa ni vile visivyojiendesha kwa kulenga faida lakini ambavyo vinatoa huduma zinazohitajika sana katika kuongeza upatikanaji wa taarifa—hasa za vijijini na maeneo yasiyofikika kwa urahisi Tanzania. Umuhimu wa redio umekuwa mkubwa, ikiwemo matangazo ya mazungumzo ya kuleta amani wakati wa uchaguzi na habari za maendeleo; kupashana habari kuhusu na kutoka serikalini na katika jamii kuhusu changamoto za mahalia zikiwemo taarifa za kujiweka tayari kwa majanga na kudhibiti milipuko ya magonjwa kama vile Ebola na Kipindupindu.

Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mh. Juliana Shonza, alitambua kazi kubwa zinayofanywa na redio za jamii. Pia alitambua na kuthamini uwakilishi katika tukio hilo uliohusisha karibu nchi nzima na aliishukuru UNESCO kwa msaada wake katika kuandaa majadiliano hayo.

Alitoa wito kwa wadau kuhakikisha wanalinda maadili na kusimamia uandishi wa habari unaojali uwajibikaji huku akiitaja Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari ya 2016 kama chombo muhimu cha kisheria kwa ajili ya maendeleo ya waandishi wa habari nchini, na ambayo inajumuisha vipengele vinavyowafunga wamiliki wa vyombo vya habari kuhakikisha wanaweka mazingira mazuri ya kufanya kazi kwa wafanya kazi wao.


Serikali ilihaidi kuendelea kushirikiana na UNESCO na wadau wa vyombo vya habari katika kuhamasisha uhuru wa vyombo hivyo na kudumisha amani. Changamoto zilibainishwa ili kufanya ufuatiliaji na Wizara itashirikiana na UNESCO na mtandao wa vyombo vya habari vya jamii ili kujumuisha kundi la tuzo kwa kituo cha redio katika Tuzo za Mwaka za Uzalendo zinazoandaliwa na Wizara.

Mapendekezo muhimu yaliyotokana na kipindi cha majadiliano ya kitaifa yanalenga kukuza ushirikiano ndani ya tasnia ya habari ili kuwa na uanuwai wa vyombo vya habari, uendelevu na uhuru wa vyombo vya habari, hasa kwa upande wa redio. Hii ilikuwa muhimu kwani nchini Tanzania, redio ni chombo chenye nguvu, kinawafikia watu wengi kuliko jukwaa lingine lolote la mawasiliano, na hivyo hutoa taarifa muhimu kuhusu masuala ya kijamii katika ngazi ya mahalia.



Mgeni rasmi katika Maadhimisho ya Siku ya Redio Duniani (WRD), Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mh. Juliana Shonza, akizungumza wakati wa majadiliano ya kitaifa kuhusu WRD huko Tanga. ***Picha | UNESCO***

## RIPOTI MAALUMU:
## Norway Yachachangia Dola Milioni 7 zaidi katika Programu ya Pamoja ya Kigoma inayolenga Kukomesha Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto




Picha zote na Edgar Kiliba/UN Tanzania

Balozi wa Norway, Mh. Elisabeth Jacobsen (kulia) akikabidhi hundi yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 7 (takribani Shilingi bilioni 16) ili kusaidia juhudi za UN katika utekelezaji wa Programu ya Pamoja ya Kigoma (KJP) na Mpango wa Taifa wa Kupambana na Vitendo vya Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto. Msaada ulipokelewa na Mratibu Mkazi wa UN, Bw. Alvaro Rodriguez (kushoto) kwa niaba ya UN nchini Tanzania. Aliyesimama kati yao ni Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Brigedia Jenerali Emmanuel Maganga, ambaye alizishukuru Norway na Umoja wa Mataifa kwa kusaidia kuleta maisha bora kwa wakazi wa mkoa wa Kigoma.

Mwishoni mwa mwezi Januari, Ubalozi wa Ufalme wa Norway ulitangaza makubaliano yake na Umoja wa Mataifa Tanzania ambapo Norway ilichangia Dola za Marekani milioni 7 (karibu sawa na Shilingi bilioni 16) kwa Umoja wa Mataifa ili kusaidia utekelezaji wa Programu ya Pamoja ya Kigoma (KJP) na Mpango wa Taifa wa Kupambana na Vitendo vya Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto. Hatua hii inafanya mchango wa Norway katika mpango kazi wa sasa wa Umoja wa Mataifa (UNDAP II) kuwa takribani Dola za Marekani milioni 20 (karibu sawa na Shilingi bilioni 47).

Makubaliano hayo yalitiwa saini rasmi Mjini Kigoma katika hafla kati ya Balozi wa Norway, Mh. Elisabeth Jacobsen, na Mratibu Mkazi wa UN, Bw. Alvaro Rodriguez. Msaada huu kutoka Norway utayawezesha mashirika ya Umoja wa Mataifa kuendelea na utekelezaji wa shughuli za KJP hasa zinazohusiana na kukomesha vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto; uwezeshaji kiuchumi wa vijana na wanawake; kuimarisha huduma za maji na usafi wa mazingira, na; kilimo kwa kuweka mkazo katika kukuza masoko ya mahalia. Kwa kuongezea, fedha hizo zitapanua msaada wa UN katika kutekeleza Mpango wa Taifa wa Kupambana na Vitendo vya Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo, Balozi wa Norway Nchini Tanzania, Mh. Elisabeth Jacobsen, alisisitiza kwamba Norway imeendelea kuwa mshirika wa Tanzania kwa zaidi ya miaka 50, ikisaidia mipango ya maendeleo katika sekta nyingi na maeneo mbalimbali ya nchi. “Katika Mkoa wa Kigoma, kumekuwa na umuhimu mkubwa kwa Norway kusaidia jamii za wenyeji ambazo zinawahifadhi wakimbizi kutoka nchi jirani za Kiafrika—tunajua kwamba jambo hili ni muhimu ili kuzuia migogoro na machafuko zaidi,” alisema. Balozi pia alisema kwamba Norway imeendelea kuwa muungaji mkono mkubwa wa UN Tanzania kupitia kanuni za

*Inaendelea ukurasa wa 7*

*Inatoka ukurasa 6*

Mpango wa Kufanya Kazi Pamoja na KJP inaendeleza dira hiyohiyo.

Bw. Rodriguez alitoa shukrani za dhati kwa serikali na watu wa Ufalme wa Norway kwa msaada wao endelevu akisema kwamba Norway imeendelea kuwa mshirika wa maendeleo asiyeyumba katika shughuli za UN na pia kwa Tanzania. “Norway imekuwa mshirika madhubuti wa Tanzania na Umoja wa Mataifa kwa miongo mingi. Imekuwa ikisaidia katika kuwanasua wanawake, watoto na vijana wanyonge, na mchango huu utakuwa na msaada wa aina yake katika kushughulikia mahitaji ya hawa ‘waliochwa nyuma zaidi’ kama inavyoelekezwa katika Malengo ya Dunia.” Vilevile, Bw. Rodriguez alisema kwamba katika miaka ijayo, UN Tanzania ina shauku ya kuimarisha zaidi ushirika wake na Norway ili kuwasaidia wanaume, wanawake na watoto wa Tanzania kufikia malengo yao kamili.

Kabla ya hafla ya kutiwa saini makubaliano, Ubalozi wa Ufalme wa Norway na Umoja wa Mataifa Tanzania walitembelea shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na mashirika ya Umoja wa Mataifa kupitia KJP katika wilaya za Kakonko, Kibondo, Kasulu na Kigoma Mjini. Maeneo ya miradi yaliyotembelewa ni pamoja na ujenzi unaoendelea wa Soko la Mpakani la Muhange lililo katika mpaka wa Tanzania na Burundi; vikundi vya vijana na wanawake ambavyo vimepata msaada kupitia KJP; na Kituo cha Maendeleo ya Jamii cha Kasanda.

Norway na UN Tanzania zimedumu katika ushirika ambao kwayo Norway imechangia Dola za Marekani milioni 16 kwa Mfuko wa Pamoja katika mzunguko wa programu ya kwanza, yaani, UNDAP I (2011-2016). Mchango wa sasa wa Norway utasaidia Mpango wa pamoja wa UN Tanzania katika mzunguko wake mpya uliozinduliwa karibuni wa UNDAP II (2016-2021).



Waandishi wa Habari Wakiwa kazini wakati wa makabidhiano ya hundi yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 7 (takribani shilingi bilioni 16) kutoka Norway kwenda Umoja wa Mataifa kwa ajili ya utekelezaji wa Programu ya Pamoja ya Kigoma (KJP) na Mpango wa Taifa wa Kupambana na Vitendo vya Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto. Waandishi hao wa habari pia walikuwa sehemu ya ujumbe uliofanya ziara katika maeneo ya miradi.

## RIPOTI MAALUMU:
## Norway Yachachangia Dola Milioni 7 zaidi katika Programu ya Pamoja ya Kigoma inayolenga Kukomesha Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto




Ujumbe ukipiga picha ya pamoja nje ya Makazi ya IOM katika Wilaya ya Kasulu ambalo ni eneo moja kuu la KJP lenye kulenga Kumaliza Vitendo vya Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto, ambalo linatekelezwa kwa ushirikiano na UNICEF, UN Women na UNFPA. IOM inaendesha makazi ya muda yaliyofunguliwa mwaka 2017 wakati wa uzinduzi wa KJP. Makazi hayo yana uwezo wa kuwasaidia hadi wanawake 20 na watoto wanaohitaji makazi salama na yanaendeshwa kwa ushirikiano na mamlaka za wilaya.




Wajumbe walipata fursa ya kutembelea baadhi ya vikundi vya vijana na wanawake ambavyo viliwakilisha wajasiriamali takribani 267 ambao wamesaidiwa na mashirika ya UNDP, ILO na UN Women chini ya Mpango wa Uwezeshaji Kiuchumi kwa Vijana na Wanawake katika Programu ya pamoja ya Kigoma. Msaada huo kwa wajasiriamali hawa unalenga kuwajengea uwezo wanawake na vijana katika kusimamia masuala ya fedha, kurasimisha biashara, upatikanaji wa mitaji na kujenga ushirikiano wa kibiashara.



Balozi wa Norway nchini Tanzania, Mh. Elisabeth Jacobsen (wa tatu kutoka kushoto) akikabidhi mabegi yasiyopitisha hewa na vitambaa visivyopitisha maji kwa mkulima kutoka Wilaya ya Kibondo. Hadi leo, mashirika ya Umoja wa Mataifa yamesambaza vifaa kwa wakulima katika wilaya tatu za Kakondo, Kibondo na Kasulu vikiwemo vitambaa visiyopitisha maji 1,355 na mabegi yasiyopitisha hewa 2,575.



Balozi wa Norway nchini Tanzania, Mh. Elisabeth Jacobsen akipokelewa na mabingwa wa jamii wa kupambana na ukatili wa kijinsia (GBV) katika Wilaya ya Kibondo. Hawa walipewa mafunzo na mashirika ya UN. Mabingwa hawa hufundishwa kuhusu madhara ya GBV katika jamii zao na wao huwa mawakala wa kuipiga vita. Hadi leo, jumla ya wanaharakati wa jamii 200 na waelimisha rika 96 wamebainishwa na wamewafikia jumla ya watu 6,853 (wanawake 4,250 na wanaume 2,603) kupitia mijadala ya wazi ya jamii na vipindi vya video vinavyokazia kupiga vita kabisa, kukataa ukatili, na kuchukua hatua kwa pamoja, kama vile kutoa taarifa kuhusu aina yoyote ya unyanyasaji wanaofanyiwa wanawake na wasichana.



Ofisa wa Ustawi wa Jamii wa Wilaya ya Kibondo, Sophia Gwamagobe (kulia), akielezea asili ya kazi yake kwa wajumbe na kusisitiza umuhimu wa mifumo ya kinga ya mtoto katika Wilaya ya Kibondo, ambao umeimarishwa kupitia ushirikiano na UNICEF, IOM, UNFPA na UN Women, ambayo kwa pamoja yanatekeleza Ujumbe Mkuu wa VAWC.



Ujumbe ulipata nafasi ya kuwasikiliza vijana ambao wameweza kupata ujuzi mbalimbali kupitia Kituo cha Maendeleo ya Jamii cha Kasanda (MPCC) kilicho nje ya Kambi ya Wakimbizi ya Mtendeli katika Wilaya ya Kakonko. Kupitia MPCC, wakazi wa eneo hilo na wakimbizi kutokana na mafunzo yanayotolewa hapo hasa kuhusu useremala, ushonaji, utengenezaji sabuni na TEHAMA.



Balozi wa Norway nchini Tanzania, Mh. Elisabeth Jacobsen (kushoto), akikabidhi vifaa vya kuhifadhia baridi maalumu kwa ajili ya chanjo ya mifumo kwa mkuu wa moja ya makundi ya wafugaji katika Wilaya ya Kakonko. Idadi ya vifaa vilivyokabidhiwa katika programu ya wilaya ina thamani ya Shilingi milioni 54,7. Vifaa hivyo vilikuwa ni pamoja na majokofu kwa ajili ya kuhifadhia chanjo, makasha ya baridi kwa ajili ya usafirishaji wa chanjo na zaidi ya dozi 370,000 za chanjo ya kudhibiti Mdondo.




Balozi wa Norway nchini Tanzania, Mh. Elisabeth Jacobsen (kushoto) na Mkuu wa Wilaya ya Kakonko, Kanali Hosea Maloda (kulia), wakiweka jiwe la msingi kwa ajili ya soko. Kibao cha jiwe hilo la msingi kinasomeka: 'Jiwe la Msingi la Soko la Mpakani la Muhange limewekwa na Mh. Elisabeth Jacobsen, Balozi wa Norway nchini Tanzania, tarehe 23 Januari, 2019'.

## WFP yatiliana saini na NFRA ili kununua tani 36,000 za mahindi



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mh. Dkt. John Pombe Magufuli akimkaribisha Mwakilishi wa Nchi wa Mpango wa Chakula Duniani (WFP), Bw. Michael Dunford, katika Ikulu ya Dar es Salaam. ***Picha | Ikulu***

Mapema mwezi Januari, Mwakilishi wa Nchi wa Mpango wa Chakula Duniani (WFP), Bw. Michael Dunford, alialikwa Ikulu na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mh. John Pombe Magufuli, kwa ajili ya hafla ya utiaji saini na Kaimu Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA), Bi. Vumilia Zikankuba, kwa ajili ya manunuzi ya tani za metriki 36,000 za mahindi. Mahindi hayo yalikuwa ni sehemu ya zaidi ya tani za metriki 160,000 za bidhaa mbalimbali za vyakula ambavyo WFP ilinunua nchini Tanzania katika mwaka 2018, na hivyo kuliingizia taifa jumla ya Dola za Marekani milioni 60 kupitia manunuzi ya bidhaa na huduma za ugavi katika kutumia korido ya Tanzania.

Wakati wa halfa hiyo, Rais aliipongeza WFP kwa kuwasaidia wakulima wadogowadogo ambao juhudi zao zinasaidia kujenga uchumi wa Tanzania. Alipongeza juhudi za WFP za kufanya biashara kwa uwazi na kuwashauri wafanyabiashara nchini kuiga mfano huo.

Nchini Tanzania, WFP inatumika kama kitovu cha masuala ya lojistiki kwa nchi zisizopakana na bahari zinazoizunguka Tanzania na ni mshirika muhimu wa ukanda wa Afrika ya Mashariki katika kuwezesha usafirishaji wa chakula kinachohitajika sana na watu wanaoishi maeneo ya migogoro na machafuko. Matumizi ya WFP ya reli ili kusafirisha chakula kutoka Dar es Salaam hadi Uganda kupitia Bandari ya Mwanza katika Ziwa Victoria ni mfano wa namna WFP inavyoweza kuhamasisha matumizi ya mnyororo wa ugavi.

Kazi za WFP zinachangia kwa kiasi kikubwa katika uchumi wa Tanania kwani inatumia makampuni ya ndani katika kushughulikia, kuhifadhi na kusafirisha chakula. Fedha zinazoingizwa katika sekta ya mnyororo wa ugavi zinakuwa na manufaa mbalimbali, kwani ajira zaidi zinatengenezwa kwa wafanyakazi na watumishi wa usafirishaji, na matokeo yake, mitaji zaidi inapatikana kwa sekta za umma na binafsi kwa ajili ya uwekezaji katika kujenga uwezo na kuimarisha miundombinu.



Mwakilishi wa Nchi wa Mpango wa Chakula Duniani (WFP), Bw. Michael Dunford (kushoto) na Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA), Bi. Vumilia Zikankuba (kulia), wakitia saini makubaliano ambapo WFP itanunua tani za metriki 36,000 za mahindi kutoka NFRA. ***Picha | Ikulu***

# Kuimarisha hatua za kupambana na vitendo vya ukatili kwa msingi wa jinsia Visiwani Zanzibar



Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto, Mh. Maudline Castico, akikabidhi vifaa vilivyotolewa na NFPA kwa Kamishna Mwandamizi Msaidizi wa Polisi, Bw. Saleh Mohd Saleh, mbele ya Bi. Halima Abdulrahman, Ofisa Mwandamizi wa Programu ya Jinsia katika Wizara hiyo. ***Picha | UNFPA***

Ingawa vinatambulika kote duniani kwamba ni ukiukwaji mkubwa kabisa wa haki za binadamu, vitendo vya ukatili kwa msingi wa jinsia (GBV) ndiyo makosa ambayo yamefikishwa mahakamani kwa idadi ndogo zaidi. Wanaohusika na kutenda makosa hayo wameendelea kufanya hivyo pasipo woga katika mazingira ambamo mitazamo ya kimila na kijamii imejichimbia mizizi na kuwaacha waathirika wengi wakiwa hawana namna ya kutafuta haki zao. Mpango wa Taifa wa Kupambana na Vitendo vya Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (NPA-VAWC), 2017-2022, wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar umeweka ahadi ya kukomesha aina zote za ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

Mfuko wa Umoja wa Mataifa wa Idadi ya Watu (UNFPA) unasaidia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee na Watoto kutekeleza NPA-VAWC. Hii inajumuisha kujenga uwezo wa polisi, ambao wako mstari wa mbele katika kupambana na vitendo vya GBV. Huko Zanzibar, UNFPA inaendelea kusaidia kuimarisha Madawati ya Jinsia na Watoto katika Vituo vya Polisi.

Madawati ya Jinsia na Watoto ni vitengo vilivyowekwa mahsusi katika Vituo vya Polisi ambapo vinafanya kazi kubwa ya kujenga uaminifu kati ya polisi na wanawake na watoto, hivyo kuandaa njia ya kupata haki ambayo haikuwapo hapo kabla.

Ili kuongeza rasilimali zilizopo kusaidia polisi kupeleleza kesi za GBV na kuwaleta waliohusika katika mkono wa sheria, Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto, kwa kutumia msaada wa kifedha kutoka UNFPA, ilinunua vifaa kwa ajili ya madawati matatu ya jinsia. Vifaa hivyo ni pamoja na kompyuta, mashine za kurudufu na samani, vyote vikiwa na thamani ya Shilingi milioni 22.7 (takribani Dola 9,870).

Akipokea vifaa hivyo kwa niaba ya Kamishna wa Polisi Zanzibar, Kamishna Mwandamizi Msaidizi wa Polisi, Bw. Saleh Mohamed Saleh, alitoa shukrani zake kwa UNFPA na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee na Watoto kwa kutambua umuhimu wa kuimarisha mazingira ya kazi ya Madawati ya Jinsia na Watoto katika Vituo vya Polisi huko Zanzibar, akiongeza kwamba hii itaongeza ufanisi katika upelelezi na kung'amua vitendo vya GBV na kuimarisha upatikanaji wa haki kwa waathirika wa vitendo vya GBV.

Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto, Mh. Maudline Castico, alisisitiza kwamba GBV lilikuwa bado ni tatizo kubwa Visiwani Zanzibar na msaada wa UNFPA unaisaidia Wizara na wadau wengine kukabiliana na tatizo hilo. Kupambana na Vitendo vya Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto ni jambo muhimu sana katika utekelezaji wa Mpango wa Pamoja wa Zanzibar (ZJP) ambao ulizinduliwa mwezi Agosti, 2018, na ambao ni ushirikiano wa kimaendeleo kati ya Umoja wa Mataifa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar

## Wanafunzi wa Tanzania waaswa kujifunza kutokana na Mauaji ya Halaiki ya Wayahudi




Naibu Balozi wa Ujerumani nchini Tanzania, Mh. Jörg Herrera (kulia) akijibu maswali kutoka kwa wanafunzi kuhusu namna Ujerumani unavyowajibika kwa vitendo vyake vya Mauaji ya Halaiki ya Wayahudi tangu baada ya kumalizika kwa mauaji hayo. Kushoto kwake ni Mratibu Mkazi wa Umoja wa Mataifa, Bw. Alvaro Rodriguez. ***Picha | UN Tanzania/Edgar Kiliba***

Kituo cha Habari cha Umoja wa Mataifa (UNIC) cha jijini Dar es Salaam kwa kushirikiana na Ofisi ya Mratibu Mkazi wa Umoja wa Mataifa na Ubalozi wa Ujerumani nchini Tanzania kiliongoza kumbukumbu za Siku ya Kimataifa ya Kuwakumbuka Waathirika wa Mauaji ya Halaiki ya Wayahudi yaliyofanyika Makumbusho ya Taifa mnamo tarehe 29 Januari, 2019.

Wanafunzi mia tatu kutoka shule za sekondari za Chang'ombe, Kibasila na Azania pamoja na wanachuo wa Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM) cha jijini Dar es Salaam walishiriki katika tukio hilo lililofunguliwa na ziara ya maonyesho iliyopewa kichwa cha habari cha 'Hali ya Udanganyifu', yaani 'State of Deception'.

Akizungumza katika tukio hilo, Naibu Balozi wa Ubalozi wa Ujerumani, Mh. Jörg Herrera, aliwasimulia wanafunzi kuhusu Mauaji ya Halaiki ya Wayahudi na jinsi Ujerumani inavyoshughulikia suala hilo na jinsi gani nchi hiyo inasaidia jitihada za kulinda Haki za Binadamu kote duniani. Bw. Herrera aliwaomba washiriki wote kuona umuhimu wa kuwakumbuka Waathirika wa Mauaji ya Halaiki ya Wayahudi na Historia ya Mauaji ya Halaiki ya Wayahudi, "Tutawakumbuka waathirika kwa sababu tunawaheshimu na tungependa kujifunza kutoka kwao, kutoka kwa Historia na pia ili kuepuka kurudia yale yaliyotokea hapo zamani. Tunakumbuka tulikotoka ili tujifunze namna ya kukabiliana na ya sasa na ya baadaye," alisema.

Mratibu Mkazi wa UN Tanzania, Bw. Alvaro Rodriguez, alisoma ujumbe maalumu kwa ajili ya siku hiyo kutoka kwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa na kuwahimiza wanafunzi kutobaguana katika jamii. "Jukumu lililo mbele yetu ni kukomesha ubaguzi na kuunga mkono jitihada zinazoimarisha misingi ya demokrasia na haki za binadamu kokote tuliko," alisema Bw. Rodriguez.



Wanafunzi kutoka shule za sekondari za Chang'ombe, Kibasila na Azania wakitazama maonyesho ya picha mbalimbali kuhusu Mauaji ya Halaiki ya Wayahudi kama yalivyoandaliwa na Kituo cha Habari cha Umoja wa Mataifa (UNIC). Tukio hilo lilipewa kichwa cha habari cha 'Hali ya Udanganyifu' ('State of Deception'). ***Picha | UN Tanzania/Edgar Kiliba***

## ILO yaandaa mafunzo kuhusu kuanzisha mnyororo wa thamani kwa kutumia Njia ya Kuanzisha Mifumo ya Masoko



Wajumbe wa Kundi la UNDAP II la Ukuaji wa Uchumi na Ukuzaji Fursa za Ajira wakishiriki mafunzo kuhusu Njia ya Kuanzisha Mifumo ya Masoko. ***Photo | ILO***

Mwishoni mwa mwezi Februari, Shirika la Kazi Duniani (ILO) liliandaa mafunzo ya siku tatu kwa maofisa wa mashirika ya Umoja wa Mataifa ambayo ni wanachama wa Kundi la Ukuaji wa Kiuchumi na Ukuzaji wa Fursa za Ajira (Economic Growth and Employment Outcome Group) la Mpango wa Msaada wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (UNDAP II) wa 2016-2021. Mashirika ya Umoja wa Mataifa katika kundi hili lenye jukumu la kuleta matokeo ni UNDP, UNCDF, UN Women, ILO, FAO, IFAD, UNIDO, ITC, UNCTAD, UNOPS, UNEP na IOM.

Mafunzo hayo yalilenga kuhamasisha uelewa wa pamoja wa dhana muhimu na njia za mnyororo wa thamani wa kuleta maendeleo kwa kutumia njia ya Uanzishaji Mifumo ya Masoko (MSD) kwa mtazamo wa kiujumla, kuimarisha uendelezaji na kupanua matokeo bora kwa ajili ya wafanyakazi maskini. Pia yalipangwa kutumika kama jukwaa na miongozo ya kuanzishwa kwa programu ya pamoja ya UN kwa ajili ya kuanzisha mnyororo wa thamani kwa ajili ya ajira ya vijana. Akizungumza kwa niaba ya ILO, Mratibu wa Economic Growth and Employment Outcome chini ya UNDAP, Bi. Kristina Weibel, aliangazia nafasi ya biashara ndogondogo, ndogo na za ngazi ya kati katika kuendeleza uchumi wa Tanzania. Vilevile, alieleza kwamba wakati ambapo kuna kukubaliana kwa jumla kuhusu umuhimu wa kuhamasiha uanzishwaji biashara ndogondogo, ndogo na za ngazi ya kati, njia zilizotumika kubuni na kutekeleza mnyororo wa thamani zilitofautiana. Hii ndiyo iliyokuwa sababu ya kutoa mafunzo hayo.

Zaidi ya wawakilishi 25 kutoka katika mashirika mbalimbali ya Umoja wa Mataifa walishiriki katika mafunzo hayo yaliyolenga katika kujenga mnyororo wa thamani kwa kutumia njia ya kimfumo ya MSD, ikiwemo uchambuzi, usanifu na utekelezaji wa jitihada za kuanzisha mifumo ya mnyororo wa thamani.

Kama mwendelezo wa mafunzo hayo, mashirika ya UN katika Kundi hilo la Matokeo watatafuta njia za kushirikiana katika kuendeleza mnyororo wa thamani kwa kutumia njia ya mifumo ya masoko. Hii ni pamoja na kuendeleza majadiliano katika kubadilishana ujuzi na kupitia miradi na programu zilizopo ili kuifanya kuchukua mwelekeo wa mifumo ya kimasoko. Vilevile, Kundi hilo la Matokeo linapanga kuandaa mafunzo kama hayo kwa ajili ya washirika ili kuhimiza njia ya kimfumo katika kuanzisha mnyororo wa thamani kwa kuimarisha taathira na upanuzi wake.

## Kuimarisha uwezo wa kitaasisi kwa ajili ya uratibu na usimamizi wa MKUZA III na SDGs huko Zanzibar

Kadiri utekelezaji wa Ajenda ya 2030 unavyoshika kasi, kuna ongezeko la mahitaji ya kuanzisha taasisi za kitaifa, mifumo, sera vyote vikiwa na ufanisi na pia kuwa na data zenye kuaminika na zenye ubora. Hili linaonyesha umuhimu wa kujenga uwezo ili kuziwezesha nchi kupanga, kutekeleza, kusimamia na kutoa taarifa kuhusu mipango yao ya maendeleo ya kitaifa kwa kuoanisha na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs). Kutokana na uwezo mdogo wa uratibu na utoaji taarifa kuhusu

*Inaendelea ukurasa wa 16*



Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango ya Zanzibar, Bw. Juma Reli, akiongoza kikao cha Kamati Ndogo ya Uongozi ya Programu ya Pamoja ya Zanzibar. ***Picha | Amalie Aase Boge/UNFPA***

***Inatoka ukurasa 15***

SDGs na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Zanzibar (MKUZA III) huko Zanzibar, ipo haja ya kuimarisha zaidi uwezo wa Zanzibar wa kuwezesha uratibu, usimamizi na utekelezaji na utoaji taarifa kuhusu SDGs na MKUZA III. Kwa kuzingatia muktadha huu, Programu ya Pamoja ya Zanzibar (ZJP) inalenga kuimarisha uwezo wa kitaasisi na kuanzisha mifumo yenye ufanisi kwa ajili ya uratibu na uongozi wa kimkakati kuhusu MKUZA III na maendeleo endelevu.

Kamati ndogo ya uongozi ya ZJP iliyo chini ya Kamati ya Uongozi ya MKUZA III tayari imeanzishwa ili: kuwezesha uwekaji mipango, usimamizi na kubaini fursa kwa kuoanisha mwitiko kati ya maeneo yanayoshughulikiwa na programu hiyo ya pamoja. Mkutano wa kwanza wa kamati ndogo uliitishwa Januari 28, 2019 katika Tume ya Mipango ya Zanzibar, chini ya uongozi wa UN na Tume ya Mipango ya Zanzibar. Ilihudhuriwa na wawakilishi kutoka ZJP, mashirika ya Umoja wa Mataifa yanayoshiriki, mashirika yanayotekeleza programu hiyo na pande nyingine zinazohusika.

Ilikubaliwa kwamba kuanzishwa kwa kamati ndogo ya uongozi lilikuwa jambo muhimu la utekelezaji wa ZJP na jukwaa sahihi la kujadili utekelezaji wa njia ya programu ya sekta nyingi katika kuleta matokeo yanayokusudiwa. Kamati ndogo ya uongozi itakutana kila robo mwaka ili kuimarisha ushirikiano katika sekta mbalimbali na kuendeleza njia ya jumla ya utekelezaji wa ZJP na Kufanya Kazi Pamoja. Mafunzo yatokanayo, kwa maana ya kupata matokeo yenye mwelekeo wa kuhusisha sekta mbalimbali, yataingizwa katika taarifa na kutumika kutoa miongozo katika utekelezaji majukumu ya MKUZA III na yatatoa mwangaza kwenye mikutano ya Kamati za Uongozi wa Wizara na Wizara (IMTC).

**Siku za Umoja wa Mataifa**

20 Machi – Siku ya Furaha Duniani

21 Machi – Siku ya Kimatifa ya Misitu

22 Machi – Siku ya Maji Duniani

24 Machi – Siku ya Kifua Kikuu Duniani

7 Aprili – Siku ya Umoja wa Mataifa ya Kutafakari Kuhusu Mauaji ya Kimbari ya Rwanda

7 Aprili – Siku ya Afya Duniani

25 Aprili – Siku ya Malaria Duniani

3 Mei – Siku ya Uhuru wa Vyombo Vya Habari Duniani

***Umoja wa Mataifa Madhubuti kwa Dunia Bora Zaidi !***



UNITED NATIONS TANZANIA

**United Nations**

**Resident Coordinator's Offce**

Phone: (+255) 22-219-5021

Website: www.tz.one.un.org

